SHERIA YA RELI,
(SURA YA 170)

---

KANUNI

---

*(Zimetengenezwa chini ya Kifungu cha 95 (2) (n))*

---

# KANUNI ZA WATOA HUDUMA BINAFSI ZA USAFIRI WA RELI ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI


Kanuni Kichwa

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MAOMBI YA LESENI NA KIBALI

4. Maombi ya kibali.
5. Ada za vibali.
6. Leseni ya kutoa huduma.
7. Ada za leseni.

SEHEMU YA TATU
UPATIKANAJI WA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA RELI

8. haki ya matumizi ya miundombinu.
9. Ufikiaji wa vituo na bandari.
10. Upatikanaji wa huduma.

SEHEMU YA NNE
USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MIUNDOMBINU

11. Uhuru wa Usimamizi.
12. Mpango wa Biashara.
13. Maelezo ya Mtandao wa Miundo mbinu.

SEHEMU YA TANO
TOZO ZA MIUNDOMBINU

14. Kuanzisha, kuamua na kukusanya tozo.
15. Mpango wa utendaji.
16. Tozo kwa miundo mbinu isiyotumika.

SEHEMU YA SITA
MGAWANYO WA MATUMIZI YA MIUNDOMBINU YA RELI

17. Mgao wa miundombinu.
18. Ratiba ya uendeshaji .
19. Kutohamishika.
20. Mgao usio na ubaguzi.
21. Kupanga na kuratibu .

22. Mkataba wa matumizi ya miundombinu.
23. Maombi ya dharula.
24. Tamko la miundombinu maalumu.
25. Msongamano wa Miundombinu .
26. Uchambuzi wa uwezo.
27. Mpango wa kuongeza uwezo.
28. Matumizi ya njia za treni.
29. Hatua maalum za kuchukuwa wakati wa dharura.
SEHEMU YA SABA
USIMAMIZI NA RUFAA
30. Chombo cha usimamizi.
31. Uwasilishaji wa malalamiko na marejeo kwa Mdhibiti.
32. Masuala ya ushindani.
33. Mamlaka ya kupata taarifa.
SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA JUMLA
34. Masharti ya leseni.
35. Uhalali wa Leseni.
36. Uchunguzi na uchambuzi wa ajali.
37. Uwajibikaji.
38. Shughuli za uokoaji.
39. Kusitishwa na kufutwa kwa leseni au kibali.
40. Matumizi na uhifadhi wa leseni au kibali.
41. Taarifa za ukiukwaji.
42. Ukaguzi wa leseni au kibali.
43. Makosa na adhabu.

---

MAJEDWALI

---

SHERIA YA RELI,

(SURA YA 170)

---

**KANUNI**

---

*(Zimetengenezwa chini ya Kifungu cha 95 (2) (n))*

KANUNI ZA KURUHUSU WATOA HUDUMA BINAFSI ZA USAFIRI
WA RELI ZA MWAKA 2023

| SEHEMU YA I<br>MASHARTI YA AWALI | |
|---|---|
| Jina | **1**.Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Watoa Huduma binafsi za Usafiri Wa Reli za Mwaka 2023 |
| | |
| Matumizi | **2**.Kanuni hizi zitatumika kwa ajili ya kuweka utaratibu na masharti katika kuruhusu watoa huduma binafsi wa usafiri wa reli kutoa huduma hiyo kwa kutumia miundombinu ya reli . |
| | |
| Tafsiri | **3**.Katika Kanuni hizi isipokuwa muktadha utahitaji vinginevyo- |
| | "mkataba wa matumizi ya miundombinu" maana yake ni makubaliano kati ya Msimamizi wa Miundombinu na Mtoa huduma inaojumuisha viambatisho na vielelezo husika; |
| | "haki ya matumizi ya miundombinu" maana yake ni haki ya kutumia miundombinu ya reli kama ilivyoombwa na Mtoa huduma; |
| | "ada ya matumizi ya miundombinu" maana yake ni ada inayoamuliwa kwa mujibu wa mkataba wa utoaji wa huduma inayolipwa kwa Msimamizi wa Miundombinu kwa ajili ya kuruhusiwa kutumia miundombinu; |
| Sura ya 170 | "Sheria" maana yake ni Sheria ya Reli. |
| | "maombi maalum" maana yake ni maombi ya kutumia njia ya treni kwa wakati maalum tofauti na ratiba ya kawaida ya mchakato wa ugawaji wa njia ya reli; |
| | "mpango wa utozaji" maana yake ni utaratibu mahususi za utozaji zilizowekwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, Mdhibiti wa Reli au msimamizi wa miundombinu kadri itakavyokuwa; |
| | "mfumo wa utozaji" maana yake ni mfumo ulioanzishwa na msimamizi wa miundombinu ili kubainisha gharama za matumizi ya miundombinu; |
| Sura ya 170 | "msimamizi wa miundombinu" maana yake ni Shirika lililoanzishwa kwa mujibu wa Sheria; |
| Sura ya 170 | "Waziri" itakuwa na maana iliyoainishwa katika Sheria; |
| | "Maelezo ya mtandao wa reli" maana yake ni maelezo yanayoonesha masharti kwa ujumla, utaratibu na vigezo vya kupanga tozo na miundombinu na ada za huduma; |
| | "mtoa huduma" maana yake ni mtu ambaye amepewa leseni na mdhibiti kutoa huduma za reli kupitia utaratibu wa kuruhu watoa huduma binafsi kutumia miundombinu ya reli; |
| | "msongamano wa treni" maana yake ni idadi kubwa ya treni zinazosafiri katika eneo moja; na |
| Sura ya 170 | "Mdhibiti" atakuwa na maana iliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria. |
| | |
| SEHEMU YA PILI | |

| MAOMBI YA KIBALI NA LESENI | |
|---|---|
| | |
| Maombi ya kibali | **4**.-(1) Mtu anayetarajia kutoa huduma za usafiri wa reli kwa utaratibu wa kuruhusu watoa huduma binafsi ataomba kibali kwa msimamizi wa miundombinu katika fomu iliyoainishwa chini ya Jedwali la Kwanza. |
| | (2) Maombi chini ya kanuni ndogo ya (1) yataambatishwa na taarifa zifuatazo- |
| | (a) taarifa ya hesabu ya fedha iliyokaguliwa karibuni; |
| | (b) uthibitisho wa wafanyakazi wa kitaaluma juu ya uendeshaji wa reli; |
| | (c) cheti cha tathmini ya athari za mazingira; |
| | (d) maombi yanayobainisha aina na kiwango cha uwezo unaohitajika katika mtandao wa reli; |
| | (e) vigezo vya usanifu wa vitendea kazi vitakavyotumika katika uendeshaji; |
| | (f) mpango wa biashara; |
| | (g) bima; |
| | (h) mfumo wa usimamizi wa usalama, mpango wa ukaguzi wa usalama na cheti cha usalama; |
| | (i) mpango wa matengenezo na miongozo ya uendeshaji; |
| | (j) lazima iwe kampuni iliyosajiliwa Tanzania; |
| | (k) utaratibu wa uthibitishaji wa madereva wa treni na moduli za mafunzo; na |
| | (l) nyaraka nyingine zozote ambazo msimamizi wa miundombinu anaweza kuhitaji. |
| | (3) Msimamizi wa Miundombinu baada ya kupokea maombi ya kibali atatoa kibali hicho ndani ya siku tisini. |
| | (4) Msimamizi wa Miundombinu anaweza kukataa kutoa kibali kwa mwombaji na atafahamisha kwa maandishi sababu za kukataa huko. |
| | (5) Baada ya maombi ya kibali kukataliwa, Mwombaji anaweza kurekebisha makosa na kuwasilisha maombi upya ndani ya siku kumi na nne. |
| | |
| Ada za vibali | **5**. Mwombaji wa kibali atalipa kwa Msimamizi wa miundombinu ada ya maombi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili ambalo linaweza kurekebishwa mara kwa mara na Mdhibiti kwa mujibu wa sheria. |
| | |
| Leseni ya kutoa huduma | **6**.-(1) Mtu hatatoa huduma za uendeshaji wa reli bila kuwa na leseni halali iliyotolewa na Mdhibiti. |
| | (2) Maombi ya leseni yatakuwa kama yalivyobainishwa kwenye jedwali la pili yakiwa na viambatisho vifuatavyo- |
| | (a) Katiba ya kampuni ya mwombaji na vifungu vya ushirika au Sheria inayoanzisha taasisi; |
| | (b) ripoti ambayo itajumuisha maelezo ya wigo wa huduma, zinazotarajiwa |

| | |
|---|---|
| | kutolewa; |
| | (c) mpango wa usalama; |
| | (d) cheti cha tathmini ya athari za mazingira; |
| | (e) tozo zinazopendekezwa; |
| | (f) muundo wa shirika ukijumuisha idadi ya wafanyakazi, uzoefu wa reli na mchanganuo wa vitengo; |
| | (g) uwezo wa kifedha wa uendeshaji biashara ya reli; |
| | (h) makubaliano na Msimamizi wa miundombinu wa utoaji wa huduma; |
| | (i) mwongozo wa dereva wa treni; |
| | (j) taratibu za kawaida za uendeshaji kwenye vituo vikubwa na karakana |
| | (k) mwongozo wa matengenezo; |
| | (l) masharti ya ubebaji; |
| | (m) wajibu na makatazo kwa abiria; |
| | (n) utaratibu wa urejeshaji wa fedha inapotokea ucheleweshaji na usitishaji wa safari; |
| | (o) usimamizi wa ushughulikiaji wa malalamiko; |
| | (p) utaratibu wa kuwahudumia walemavu na wasiojiweza kwenye treni; |
| | (q) nakala iliyothibitishwa ya kibali kilichotolewa na msimamizi wa miundombinu; |
| | (r) Uthibitisho wa malipo kwa Mdhibiti ya ada za maombi ya Leseni; na |
| | (s) nyaraka nyingine zozote ambazo zinaweza kusaidia upatikanaji wa leseni kama inavyoweza kutakiwa na Mdhibiti. |
| | (3) Mdhibiti baada ya kupokea maombi ya leseni atatoa leseni ndani ya siku ishirini na moja. |
| | (4) Mdhibiti anaweza kukataa kutoa leseni kwa mwombaji na atamjulisha mwombaji kwa maandishi sababu za kukataliwa huko. |
| | (5) Baada ya maombi ya leseni kukataliwa, Mwombaji anaweza kurekebisha makosa na kuwasilisha maombi upya ndani ya siku kumi na nne. |
| | |
| Ada za leseni | **7**. Baada ya Maombi ya leseni kukubaliwa, mtoa huduma atapaswa kulipa ada za leseni kwa Mdhibiti kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Pili. |
| | |
| SEHEMU YA TATU<br>UPATIKANAJI WA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA RELI | |
| | |
| Haki ya matumizi ya miundombinu | **8**. Mtoa huduma ana haki sawa ya kutumia mindombinu kwa ajili ya uendeshaji katika aina yoyote ya njia ya reli. |

| | |
|---|---|
| | |
| Ufikiaji wa vituo na bandari | **9**.-(1) Mtoa huduma ana stahili, kwa madhumuni ya uendeshaji wa reli, kufuatilia upatikanaji wa huduma katika vituo na bandari zilizounganishwa na mtandao wa reli zinazohudumia mtumiaji zaidi ya mmoja. |
| | (2) Msimamizi wa Miundombinu, atahakikisha kwamba stahili zinazotolewa na Kanuni hizi zinaheshimiwa, na kwamba ufikiaji na utoaji wa huduma unatolewa kwa njia ya uwazi na isiyobagua. |
| | |
| Upatikanaji wa huduma | **10**.-(1) Mtoa huduma ana haki ya kupata huduma zinazojumuisha- |
| | (a) kiwango cha chini cha huduma ya miundombinu kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu. |
| | (b) ufikiaji wa vifaa vya huduma na usambazaji wa huduma kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu |
| | (2) Endapo Msimamizi wa Miundombinu ambaye ombi limepelekwa kwake kuhusu utoaji wa huduma iliyorejewa katika aya ya 2 ya Jedwali la Tatu hatoi huduma hiyo, Msimamizi wa Miundombinu atatumia juhudi zote zinazofaa kuwezesha upatikanaji wa huduma hiyo. |
| | (3) Endapo Msimamizi wa Miundombinu atajitolea kutoa huduma za ziada kwa mujibu wa Kanuni hizi kwa kujibu ombi kutoka kwa mwombaji, atatoa huduma hiyo kulingana na upatikanaji; |
| | (4) Mwombaji anaweza kuomba kupatiwa huduma zilizoainishwa katika aya ya 2 ya Jedwali la Tatu au huduma za ziada kutoka kwa Msimamizi wa Miundombinu ingawa Msimamizi wa Miundombinu hatalazimika kukubali maombi hayo; |
| | (5) Bila ya kuathiri ujumla masharti ya Kanuni hizi, mtoa huduma ambaye amekataliwa haki aliyopewa na kanuni hii anaweza kukata rufaa kwa Mdhibiti. |
| | |
| SEHEMU YA NNE<br>USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MIUNDOMBINU | |
| | |
| Uhuru wa Usimamizi | **11**. Mtoa huduma atadumisha hadhi ya mwendeshaji huru katika usimamizi wa shughuli zake za kutoa huduma ya reli.. |
| | |
| Mpango wa Biashara | **12**.-(1) Msimamizi wa Miundombinu atatengeneza mpango wa biashara ambao umeundwa kwa madhumuni ya kuhakikisha- |
| | (a) matumizi bora,thabiti na uendelezaji wa miundombinu; na |
| | (b) uwezo wa kifedha. |
| | (2) Mpango wa Biashara utajumuisha maelezo ya mipango ya uwekezaji na fedha, na kutoa njia ambazo malengo yaliyowekwa yatafikiwa. |
| | (3) Mtoa huduma atatengeneza mpango wa biashara unaojumuisha uwekezaji na mipango yake ya ufadhili, na ambao umeundwa kwa madhumuni ya kuhakikisha- |
| | (a) uwezo wa kifedha; na |
| | (b) malengo mengine ya kiufundi, biashara na usimamizi wa fedha. |
| | (4) Mpango wa biashara utatoa njia za kufikia malengo yaliyowekwa |

| | |
|---|---|
| | katika kanuni ndogo ya (3). |
| | (5) Msimamizi wa Miundombinu na Mtoa Huduma, watawasilisha mpango wa biashara kila mwaka kwa Mdhibiti na ripoti ambayo itaainisha matakwa ya Kanuni hizi. |
| | |
| Maelezo ya mtandao wa miundo mbinu | **13**.-(1) Msimamizi wa Miundombinu ndani ya mwezi mmoja baada ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi atashauriana na wahusika wote na kuandaa maelezo ya mtandao wa miundombinu. |
| | (2) Maelezo ya mtandao wa miundombinu yatakuwa na taarifa zifuatazo- |
| | (a) sehemu inayoelezea sifa ya miundombinu ya reli ambayo inapatikana kwa waombaji na masharti ya kuipata; |
| | (b) maelezo ya taarifa zaidi ambayo yanaweza kupatikana kuhusu sifa ya njia, na utoaji wa huduma katika vituo, bandari na vifaa vya huduma kwa mujibu wa Kanuni hizi; |
| | (c) ufafanuzi wa miongozo ya malipo na tozo, ikiwa ni pamoja na maelezo ya mbinu ya malipo, isipokuwa kwa kanuni za malipo na punguzo; |
| | (d) maelezo ya gharama za utoaji wa huduma hizo zitaorodheshwa. |
| | (e) maelezo ya kanuni na vigezo vya ugawaji wa uwezo wa miundombinu, kuweka sifa za jumla za uwezo wa miundombinu inayopatikana na vikwazo vya matumizi yake, ikiwa ni pamoja na mahitaji ya uwezo wa matengenezo; na |
| | (f) utaratibu na tarehe za mwisho katika mchakato wa ugawaji wa uwezo na vigezo maalum vilivyotumika katika mchakato huo ambavyo ni pamoja na- |
| | (i) taratibu ambazo waombaji wanaweza kuomba uwezo wa miundombinu kutoka kwa Msimamizi wa Miundombinu; |
| | (ii) taarifa inayotolewa na waombaji; |
| | (iii) ratiba ya maombi na mchakato wa ugawaji; |
| | (iv) utaratibu wa utatuzi wa migogoro ulioanzishwa na msimamizi wa miundombinu katika kutatua migogoro inayohusu ugawaji wa uwezo wa miundombinu ya reli; |
| | (v) maelezo kuhusu sehemu ya miundombinu ya reli ambayo imetengwa kwa matumizi maalum ya huduma za reli; |
| | (vi) utaratibu unazopaswa kufuatwa kwa miundombinu yenye msongamano, na vigezo vyovyote vya kipaumbele vya ugawaji wa miundombinu yenye msongamano vilivyowekwa kwa mujibu wa Kanuni hizi; |

| | |
|---|---|
| | |
| | (vii) matokeo ya mpango wowote wa kukuza uwezo uliokamilishwa kwa mujibu wa Kanuni hizi; |
| | (viii) maelezo ya makatazo juu ya matumizi ya miundombinu; |
| | (ix) kiwango cha kizingiti kitakachotumiwa na Msimamizi wa Miundombinu katika kuhitaji njia ya treni kuirudisha; |
| | (x) masharti yanayohusu viwango vya awali vya matumizi ya uwezo yazingatiwe na Msimamizi wa Miundombinu katika kuamua vipaumbele;na |
| | (xi) hatua zinazochukuliwa na Msimamizi wa Miundombinu ili kuhakikisha kuwa kunatendewa haki kwa waendeshaji mtandao na katika kujibu maombi maalum ya uwezo wa miundombinu. |
| | (3)Mtoa huduma atampa msimamizi wa miundombinu taarifa kama inavyohitajika ili kuwezesha msimamizi wa miundombinu- |
| | (a) kujumuisha maelezo juu ya hali ya upatikanaji wa njia, usambazaji wa huduma, vituo na vifaa ambavyo vinaweza kupatikana; na |
| | (b) sasisha maelezo ya mtandao. |
| | (4) Ikiwa Msimamizi wa Miundombinu hajaridhika na taarifa iliyowasilishwa na mtoa huduma, atamtaka mtoa huduma kuwasilisha tena taarifa za kutosha. |
| | (5) Msimamizi wa Miundombinu atasasisha taarifa ya mtandao na kuirekebisha inapohitajika. |
| | (6) Msimamizi wa Miundombinu katika kila mwaka wa fedha atatayarisha taarifa ya mtandao si chini ya miezi minne kabla ya tarehe ya mwisho ya kutuma maombi ya matumizi ya miundombinu kama ilivfofafanuliwa kwenye ratiba ya maombi na hatua za ugawaji. |
| | |
| SEHEMU YA TANO<br>TOZO ZA MIUNDOMBINU | |
| Kuanzisha, kuamua na kukusanya tozo | **14**.-(1)Msimamizi wa Miundombinu atatakiwa- |
| | (a) kupendekeza tozo zitakazotozwa kwa ajili ya matumizi ya miundombinu zitakazozingatia mfumo wa malipo, sheria na kanuni zilizoainishwa katika Jedwali la Nne la knuni hizi; na |
| | (b) kukusanya tozo hizo. |
| | (2) Mdhibiti ataamua utaratibu wa kutoza na miongozo mahususi inayosimamia maamuzi ya utozaji. |
| | (3) Mwombaji atalipa ada atakazotozwa na Msimamizi wa Miundombinu kwa matumizi ya miundombinu ya reli. |
| | (4) Msimamizi wa miundombinu atawasilisha taarifa kuhusu gharama za matumizi ya miundombinu kwa Mdhibiti pale inapohitajika. |
| | (5) Msimamizi wa miundombinu ataheshimu usiri wa kibiashara wa |

| | |
|---|---|
| | taarifa zinazotolewa kwake na waombaji kuhusu uwezo wa uendeshaji. |
| | |
| Mpango wa utendaji | **15.-(**1) Msimamizi wa Miundombinu ataanzisha mpango wa utendaji kama sehemu ya mfumo wa utozaji ili kuwahimiza watoa huduma na Msimamizi wa Miundombinu kupunguza usumbufu na kuboresha utendaji wa mtandao wa reli. |
| | (2) Mpango wa utendaji unaweza kujumuisha- |
| | (a) adhabu kwa vitendo vinavyovuruga uendeshaji wa mtandao wa reli; |
| | (b) fidia kwa biashara ambayo inakabiliwa na usumbufu; na |
| | (c) malipo ya ziada yanayotolewa kwa utendaji uliovuka malengo. |
| | (3) Miongozo ya msingi ya mpango wa utendaji zitatumika kwa njia isiyo ya kibaguzi katika mtandao wote ambao mpango huo unahusika. |
| | |
| Tozo kwa miundo mbinu isiyotumika | **16**. Msimamizi wa Miundombinu anaweza kutoza tozo atakayoona inafaa kwa uwezo ulioombwa na kutotumika, na atatoa motisha kwa matumizi bora ya uwezo. |
| | |
| SEHEMU YA SITA<br>MGAWANYO WA MATUMIZI YA MIUNDOMBINU YA RELI | |
| Mgao wa miundombinu | **17**.-(1) Mwombaji anaweza kutuma maombi ya mgao wa matumizi ya miundombinu kwa msimamizi wa miundombinu. |
| | (2) Msimamizi wa Miundombinu ataweka utaratibu mahususi wa mgao wa matumizi ya miundombinu. |
| | (3) Msimamizi wa Miundombinu atashughulikia maombi ya mgao wa matumizi ya miundombinu ndani ya siku kumi na nne za kazi baada ya kuwasilisha maombi. |
| | (4) Msimamizi wa Miundombinu hatagawa matumizi ya miundombinu kwa njia mahususi za treni kwa kipindi chochote kinachozidi muda wa ratiba ya kazi. |
| | (5) Mkataba au aina yoyote ya makubaliano unaoweka haki na wajibu wa wahusika, unatakiwa kuingiwa kati ya msimamizi wa miundombinu na mwombaji yeyote ambaye ameruhusiwa kutumia miundombinu ya reli kabla hajaanza kutumia miundombinu hiyo. |
| | (6) Msimamizi wa miundombinu atazingatia nafasi iliyowekwa na mtoa huduma katika kuhifadhi mgao wa matumizi ya miundombinu kwa madhumuni ya matengenezo ya njia yaliyopangwa. |
| | |
| Ratiba ya uendeshaji | **18**.-(1) Msimamizi wa Miundombinu ataandaa ratiba ya uendeshaji mara moja kwa mwaka wa kalenda. |
| | (2) Ratiba ya uendeshaji iliyorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) inaweza kupitiwa upya mara kwa mara kadiri itakavyohitajika au pale msimamizi wa miundombinu atakapoona inafaa. |
| | |
| Kutohamishika | **19.-(**1) Mwombaji ambaye amepewa mgao wa matumizi ya miundombinu na Msimamizi wa Miundombinu hatabadilisha nafasi hiyo na mwombaji mwingine au kuihamisha kwa mtoa huduma mwingine, iwe nafasi hiyo ni ya-- |
| | (a) makubaliano yaliyofanywa kwa mujibu wa Kanuni hizi; au |

(b) uwezo maalum wa miundombinu katika mfumo wa njia ya treni

(2) Mtu anayekiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) hataruhusiwa kuomba mgao wa matumizi ya miundombinu kwa muda wa mwaka mmoja.

Mgao usio na ubaguzi

**20**. Msimamizi wa Miundombinu atahakikisha kwamba mgao wa matumizi ya miundombinu unatolewa kwa misingi ya haki na isiyo ya ubaguzi na mkataba unaoingia ni wa uwazi na kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni hizi.

Kupanga na kuratibu

**21.-(**1) Msimamizi wa Miundombinu atashughulikia maombi yote ya mgao wa matumizi ya miundombinu na kuzingatia vikwazo vyote kwa waombaji, ikiwa ni pamoja na athari za kiuchumi kwenye biashara zao.

(2) Msimamizi wa Miundombinu anaweza kutoa kipaumbele kwa huduma mahususi ndani ya mchakato wa kuratibu kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(3) Msimamizi wa Miundombinu atashauriana na wahusika kuhusu rasimu ya ratiba ya uendeshaji na Msimamizi wa Miundombinu atatoa kwa wahusika hao angalau mwezi mmoja kuwasilisha maoni yao.

(4) Endapo kuna mgongano kati ya maombi tofauti ya uwezo wa miundombinu, Msimamizi wa Miundombinu, kwa kushauriana na waombaji husika, na kupitia uratibu wa maombi, atapendekeza mgao mbadala wa matumizi ya miundombinu kutoka ule ulioombwa ili kutatua mgogoro.

(5) Msimamizi wa Miundombinu atawezesha uanzishaji na uendeshaji wa mfumo wa ndani wa utatuzi wa migogoro ili kutatua migogoro ya mgao wa matumizi ya miundombinu.

(6) Msimamizi wa Miundombinu atachukua hatua zinazofaa ili kushughulikia masuala yoyote kuhusu mchakato wa mgao wa matumizi ya miundombinu uliotolewa na wahusika.

(7) Kwa madhumuni ya kanuni hii "wahusika wenye nia" ni pamoja na-

(a) waombaji wote wa mgao wa matumizi ya miundombinu kama sehemu ya mchakato maalum wa ugawaji ambao rasimu ya ratiba ya uendeshaji inahusiana; na

(b) Wadau ambao wameonesha kwa Mdhibiti nia yao ya kujadili rasimu ya ratiba ya uendeshaji.

Mkataba wa matumizi ya miundombinu

**22**.-(1) Mwombaji ambaye ni sehemu ya makubaliano ya mkataba wa matumizi ya miundombinu anaweza kuomba kupatiwa mgao wa matumizi ya miundombinu kwa mujibu wa masharti ya makubaliano hayo.

(2) Mkataba wa matumizi ya miundombinu hautazuia matumizi ya miundombinu ya reli kwa watoa huduma wengine.

(3) Mkataba wa matumizi ya miundombinu utakuwa na masharti yanayoruhusu marekebisho au ukomo wa masharti yoyote yaliyomo katika makubaliano hayo ili kuwezesha matumizi bora ya miundombinu ya reli.

(4) Mkataba wa matumizi ya miundombinu utaweka adhabu zinazotumika katika kurekebisha au kusitisha makubaliano na upande wowote.

(5) Mkataba wa matumizi ya miundombinu kwa mujibu wa Kanuni hizi hautazidi muda wa miaka mitano na unaweza kuhuishwa.

(6) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (5), mkataba wa matumizi ya miundombinu unaweza kuwa wa muda wa zaidi ya miaka mitano

katika mazingira ya kipekee hasa pale ambapo kuna uwekezaji mkubwa na wa muda mrefu ambapo uwekezaji huo unafungamana na masharti ya kimkataba.

Maombi ya dharula

**23.-(**1) Mtoa huduma anaweza kuwasilisha maombi ya dharura ya uwezo wa miundombinu katika mfumo wa njia za treni kwa msimamizi wa miundombinu.

(2) Msimamizi wa Miundombinu atajibu maombi hayo ndani ya siku tano za kazi kuanzia tarehe ya kupokea maombi.

(3) Msimamizi wa Miundombinu atahakikisha kwamba taarifa juu ya mtandao wa reli wa akiba zinapatikana kwa watoa huduma wote.

(4) Msimamizi wa Miundombinu atahakikisha uwepo wa uwezo wa akiba utakaowekwa wakati wa ratiba ya mwisho ya kazi ili kumuwezesha kujibu haraka kwa kile kinachotarajiwa.

Tamko la miundombinu maalumu

**24**. Msimamizi wa Miundombinu anaweza kutenga sehemu fulani za miundombinu kwa ajili ya matumizi ya aina maalum za huduma ya reli na, mara tu miundombinu itakapotengwa, anaweza kutoa kipaumbele kwa aina hiyo maalum ya huduma ya reli katika mgao wa miundombinu.

Msongamano wa Miundombinu

**25.-(**1) Endapo itashindikana kukidhi maombi ya uwezo, baada ya kushauriana na waombaji, msimamizi wa Miuondombinu atatoa tamko kwanini maombi hayo hayawezi kutekelezwa.

(2) Katika utayarishaji wa ratiba ya kazi, msimamizi wa miundombinu akiona dalili ya miundombinu kusongamana katika kipindi kinachohusiana na ratiba ya kazi, msimamizi wa miundombinu atatoa tamko juu ya dalili hizo.

(3) Wakati miundombinu imetangazwa kuwa na msongamano chini ya masharti ya kanuni hii msimamizi wa miundombinu atawajulisha -

(a) watumiaji waliopo;

(b) waombaji wapya, na

(c) Mdhibiti.

(4) Miundombinu inapotangazwa kuwa na msongamano, msimamizi wa miundombinu atafanya uchambuzi wa uwezo wa miundombinu yenye msongamano, isipokuwa kama mpango wa uimarishaji uwezo uko katika mchakato wa kutekelezwa.

(5) Ikiwa tamko la miundombinu iliyosongamana limetolewa, lakini tatizo la msongamano likatatuliwa kabla ya uchambuzi wa uwezo wa miundombinu kukamilika, msimamizi wa miundombinu anaweza kubatilisha tamko la msongamano lililotolewa chini ya kanuni hii na atawajulisha watumiaji waliopo, waombaji wapya na Mdhibiti wa reli.

Uchambuzi wa uwezo

**26**. (1) Pale ambapo kuna msongamano, msimamizi wa miundombinu atafanya uchambuzi wa uwezo wa miundombinu iliyosongamana ili kubaini sababu za msongamano huo na hatua za kuchukua ili kutatua msongamano huo.

(2) Katika kufanya uchambuzi wa uwezo, Msimamizi wa Miundombinu atazingatia-

(a) sifa za miundombinu iliyosongamana;

(b) taratibu za uendeshaji zinazotumika kwenye miundombinu hiyo; na

(c) sifa za huduma mbalimbali za reli zilizopewa uwezo wa kufanya kazi kwenye miundombinu hiyo.

(3) Wakati wa kutatua msongamano, Msimamizi wa Miundombinu atazingatia-

(a) upangaji upya wa huduma;

(b) kupanga upya muda wa huduma;

(c) mabadiliko ya mwendokasi, na

(d) uboreshaji wa miundombinu.

(4) Msimamizi wa miundombinu atakamilisha uchambuzi wa uwezo ndani ya mwezi mmoja kuanzia tarehe ambayo miundombinu imetangazwa kuwa na msongamano na kutoa matokeo ya uchambuzi kwa watoa huduma waliopo, waombaji wapya na Mdhibiti.

Mpango wa kuongeza uwezo

**27**.-(1) Msimamizi wa Miundombinu, atatayarisha mpango wa kuongeza uwezo wa miundombinu ndani ya mwezi mmoja baada ya kukamilisha uchambuzi.

(2) Katika kuandaa mpango wa kukuza uwezo, Msimamizi wa Miundombinu atashauriana na wadau wakiwemo watoa huduma waliopo, waombaji wapya na Mdhibiti.

(3) Mpango wa kuongeza uwezo utajumuisha-

(a) uwezekano wa ukuaji wa usafirishaji kwa siku zijazo;

(b) vikwazo katika maendeleo ya miundombinu;

(c) chaguo na gharama za kuongeza uwezo, pamoja na athari zinazoweza kujitokeza;

(d) maelezo ya hatua zitakazochukuliwa ili kuongeza uwezo wa miundombinu yenye msongamano kwa kuzingatia uchambuzi wa faida na gharama; na

(e) ratiba ya kukamilisha hatua za kina zilizoainishwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (d).

(4) Mwezi mmoja baada ya kukamilika kwa uchambuzi wa uwezo, Msimamizi wa Miundombinu atawapa wahusika alioshauriana nao chini ya kanuni ndogo ya (2), nakala ya mpango na ratiba ya kukamilisha hatua zilizoainishwa ili kutatua msongamano.

Matumizi ya njia za treni

**28**.-(1) Pale ambapo miundombinu imetangazwa kuwa na msongamano, Msimamizi wa Miundombinu atamtaka mtoa huduma ambaye, kwa kipindi cha angalau mwezi mmoja, ametumia njia ya treni mara chache kuliko kiwango kilichoainishwa katika taarifa ya mtandao, kusalimisha njia hiyo ya treni.

(2) Masharti ya kanuni ndogo (1) hayatatumika endapo kwa mujibu wa Msimamizi wa Miundombinu itaonekana kuwa mtoa huduma ameshindwa kutumia njia ya reli kwa kiwango kilichoainishwa katika taarifa ya mtandao kutokana na sababu

| | |
|---|---|
| | zisizo za kiuchumi ambazo ziko nje ya uwezo wa mtoa huduma. |
| | (3) Msimamizi wa Miundombinu anaweza, katika taarifa ya mtandao kubainisha masharti ambayo viwango vya awali vya matumizi ya uwezo vitazingatiwa ili kuonyesha vipaumbele wakati wa kufanya maamuzi kuhusu ugawaji. |
| | |
| Hatua maalum za kuchukuwa wakati wa dharura | **29**.-(1) Msimamizi wa Miundombinu atachukua hatua zinazohitajika kurejesha utendaji kazi wa kawaida wa mtandao wa reli baada ya kutokea hitilafu kwenye njia ya treni iliyosababishwa na tatizo la kiufundi au ajali. |
| | (2) Msimamizi wa Miundombinu atakuwa na mpango wa dharura wa kushughulikia usumbufu mkubwa wa usafiri wa treni. Mpango huo utaonyesha wadau wakuu ambao wanatakiwa kufahamishwa kuhusu tukio hilo. |
| | (3) Pale inapotokea dharura itakayosababisha kufungwa kwa muda sehemu ya miundombinu, Msimamizi wa Miundombinu anaweza, bila taarifa kusitisha njia za reli zilizotengwa kwa muda ili kukarabati miundombinu iliyoathirika. |
| | (4) Msimamizi wa Miundombinu anaweza kuhitaji watoa huduma kutumia rasilimali ambazo zinafaa kurejesha utendakazi wa kawaida wa mtandao. |
| | (5) Pale ambapo mkataba wa matumizi ya miundombinu kati ya mtoa huduma na msimamizi wa miundombinu unajumuisha masharti kuhusu hatua maalum zinazopaswa kuchukuliwa endapo kutatokea usumbufu, rasilimali zinazohitajika na msimamizi wa miundombinu chini ya kanuni ndogo ya (4) zitazingatia masharti hayo. |
| | |

**SEHEMU YA VI**

**UDHIBITI NA RUFAA**

| | |
|---|---|
| Chombo cha usimamizi | **30**.-(1) Upatikanaji na usimamizi wa miundombinu ya reli utakuwa chini ya uangalizi wa Mdhibiti. |
| | (2) Msimamizi wa Miundombinu atahakikisha kwamba tozo za matumizi ya miundombinu ya reli zinazingatia matakwa ya kanuni hizi. |
| | (3) Msimamizi wa Miundombinu atawasilisha kwa Mdhibiti taarifa ya mtandao reli kwa ajili ya kuidhinishwa, mpango wa ugawaji wa uwezo, utaratibu na mfumo wa tozo, muundo wa ada za miundombinu na ukokotoaji utakaofanywa ili kufikia mapendekezo ya ada na mipango mingine yoyote kuhusiana na haki ya upatikanaji iliyotolewa. |
| | |
| Uwasilishaji wa malalamiko na marejeo kwa Mdhibiti | **31**.-(1) Endapo mtoa huduma anaamini kuwa hajatendewa haki, kubaguliwa au kutokuridhishwa na maamuzi yaliyotolewa na Msimamizi wa Miundombinu, anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa Mdhibiti. |
| | (2) Taratibu za kushughulikia malalamiko kama ilivyoainishwa na Mdhibiti zitatumiwa na watoa huduma kuwasilisha malalamiko dhidi ya Msimamizi wa Miundombinu. |
| | (3) Baada ya kupokea malalamiko Mdhibiti anaweza- |
| | (a) kuthibitisha uamuzi wa msimamizi wa miundombinu; au |
| | (b) kubadilisha maamuzi au maagizo yaliyotolewa na msimamizi wa mindombinu. |
| | |
| Masuala ya ushindani | **32.** Mdhibiti atawajibika kukuza ushindani wa haki katika huduma za reli na kuzuia vitendo vinavyokiuka misingi ya ushindani katika soko la huduma za reli. |
| | |

| | |
|---|---|
| Mamlaka ya kupata taarifa | **33**. Mdhibiti atakuwa na mamlaka ya kupata taarifa zinazohusiana na majukumu na kazi zake kutoka kwa Msimamizi wa Miundombinu, watoa huduma, na wadau wengine husika. |
| | |
| SEHEMU YA VII<br>MASHARTI YA JUMLA | |
| | |
| | |
| Masharti ya leseni | **34**. Kwa kuzingatia Kanuni hizi, mtoa huduma atahakikisha kwamba- |
| | (a) hakuna mabadiliko ya shughuli au udhibiti bila ridhaa ya Mdhibiti; |
| | (b) kuna matengenezo sahihi ya mfumo wa taarifa za Usimamizi ili kufuatilia utendaji na maendeleo ya huduma za reli; |
| | (c) taarifa zinazotolewa katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi zinawasilishwa kila mwezi au kwa vipindi vingine vilivyoainishwa na Mdhibiti mara kwa mara; |
| | (d) sehemu ya uhasibu katika Mfumo wa Taarifa za Usimamizi haikinzani na sheria za Jamhuri ya Muungano; |
| | (e) ndani ya miezi sita ya kila mwaka wa fedha kuwasilisha kwa Mdhibiti taarifa utendaji kazi na hali ya kifedha kutoka kwa mkaguzi huru. |
| | |
| Uhalali wa Leseni | **35**. Leseni ya utendaji kazi wa reli itakuwa halali kwa muda wa miaka mitano kuanzia tarehe ya kutolewa, isipokuwa kama itafutwa au kusitishwa kwa mujibu wa masharti yoyote katika Kanuni hizi:<br>Isipokuwa, mtoa huduma anaweza kuhuisha leseni baada ya kuridhika na matakwa ya Kanuni hizi. |
| | |
| Uchunguzi na uchambuzi wa ajali | **36. -**(1) Inapotokea ajali, uchunguzi na uchambuzi utafanywa na Msimamizi wa Miundombinu na mtoa huduma kwa pamoja. |
| | (2) Ili kuzuia kutokea kwa ajali Msimamizi wa Miundombinu na mtoa huduma wataridhia kwa pamoja maazimio ya ripoti ya ajali. |
| | (3) Pale ambapo chanzo cha ajali hakijathibitishwa na wahusika au pale ambapo maafikiano hayajafikiwa kati ya mtoa huduma na Msimamizi wa Miundombinu kuhusu chanzo cha ajali, mdhibiti atachunguza ajali hiyo na taarifa yake itakuwa na maamuzi ya mwisho kuhusu chanzo cha ajali. |
| | |
| Uwajibikaji | **37.** Uchunguzi utakapokamilika, aliyesababisha ajali atawajibika kulipa fidia ndani ya siku sitini tangu tarehe ya kukamilika kwa uchunguzi. |
| | |
| Shughuli za uokoaji | **38.-**(1) Katika tukio la ajali inayohusisha treni ya mtoa huduma, kazi za uokoaji na kurejesha shughuli za uendeshaji zitafanywa na msimamizi wa miundombinu kwa mujibu wa mipango ya dharura na itakuwa katika gharama za ziada. |
| | |
| Kusitishwa na kufutwa kwa leseni au kibali | **39**.-(1) Mdhibiti au Msimamizi wa Miundombinu, anaweza, kumuamuru mtoa huduma kurekebisha mapungufu ya kiutendaji na masharti yoyote ambayo |

| | |
|---|---|
| | yamekiukwa. |
| | (2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), pale ambapo mtoa huduma atashindwa kurekebisha hitilafu hiyo au ukiukaji wa masharti yoyote, Mdhibiti atasimamisha au kufuta leseni baada ya kushauriana na Msimamizi wa Miundombinu na Waziri. |
| | (3) Msimamizi wa Miundombinu anaweza kumsimamisha mtoa huduma wa reli kwa zaidi ya miezi kumi na mbili, ikijumuisha sababu zifuatazo- |
| | (a) ikiwa mtoa huduma ataacha kutoa huduma za treni kwa mujibu wa masharti ya leseni kwa muda wa wiki nne, bila taarifa rasmi kwa Mdhibiti; |
| | (b) ikiwa mtoa huduma hakidhi viwango vinavyohitajika au uwezo wa kufanya kazi; |
| | (c) ikiwa mtoa huduma amefilisika; |
| | (d) ikiwa mtoa huduma ameshindwa kurekebisha mapungufu ndani ya muda aliopewa; au |
| | (e) mtoa huduma amekiuka masharti ya leseni; |
| | (4) Mdhibiti anaweza kufuta leseni ya kuendesha reli au kibali baada ya notisi ya miezi miwili kwa moja ya sababu zifuatazo- |
| | (a) mtoa huduma akishindwa kuanza kazi ndani ya miezi sita kuanzia tarehe ya leseni au kibali kutolewa; |
| | (b) ikiwa mtoa huduma ametoa taarifa za uongo katika maombi ya leseni au kibali; |
| | (c) ikiwa mtoa huduma atashindwa kutii amri inayomtaka kurekebisha masharti ya leseni au kibali ndani ya miezi mitatu kuanzia tarehe aliyopewa notisi; |
| | (d) ikiwa kuna mabadiliko ya umiliki wa mtoa huduma; |
| | (e) ikiwa Msimamizi wa Miundombinu ametoa notisi ya kusitisha mkataba. |
| | |
| Matumizi na uhifadhi wa leseni au kibali | **40**.-(1) Mtu hataruhusiwa- |
| | (a) kutumia leseni yoyote, cheti, kibali au idhini au hati nyingine iliyotolewa au inayohitajika chini ya Kanuni hizi ambayo imeghushiwa, kubadilishwa, kubatilishwa, au kusimamishwa, au ambayo mtu huyo hastahili; |
| | (b) kughushi au kubadilisha leseni, kibali, idhini au hati nyingine yoyote iliyotolewa au kuhitajika chini ya Kanuni hizi; |
| | (c) kuazimisha leseni, kibali, idhini au hati nyingine yoyote iliyotolewa au inayohitajika chini ya Kanuni hizi kwa mtu mwingine; au |
| | (d) Kulaghai kwa madhumuni ya kujipatia leseni, kibali, idhini au hati nyingine yoyote. |

| | |
|---|---|
| | (2) Mtu hatadhamiria kutoa leseni yoyote, kibali au idhini au hati nyingine yoyote kwa madhumuni ya Kanuni hizi isipokuwa kama ameidhinishwa kufanya hivyo chini ya Kanuni hizi. |
| | |
| Taarifa za ukiukwaji | **41.-**(1) Mtu mwenye taarifa ya ukiukwaji wa Sheria, Kanuni au amri yoyote iliyotolewa chini yake, atamtaarifu Mdhibiti. |
| | (2) Mdhibiti ataamua aina ya uchunguzi wa ziada au hatua zitakazochukuliwa. |
| | |
| Ukaguzi wa leseni au kibali | **42**. Mdhibiti au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa na Mdhibiti anaweza kuamuru mtu mwenye leseni, kibali au idhini chini ya kanuni hizi kuwasilisha kwa ajili ya ukaguzi. |
| | |
| **SEHEMU YA VIII**<br>**MAKOSA NA ADHABU** | |
| Makosa na adhabu | **43**.-(1) Mtu anayekiuka masharti yoyote ya Kanuni hizi anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na isiyozidi shilingi milioni mia moja au kifungo kisichopungua miaka miwili jela na isiyozidi miaka mitano jela au vyote kwa pamoja. |
| | (2) Ikiwa ukiukwaji wa sheria au kanuni utaendelea, kila siku ya uvunjaji huo itakuwa ni kosa tofauti na atatozwa faini ya ziada isiyopungua shilingi milioni tano kwa kila siku kosa likiendelea. |
| | (3) Iwapo itathibitika kwamba kitendo au kutotenda kwa mtu yeyote, jambo ambalo lingekuwa ni ukiukwaji wa masharti ya Kanuni, amri au notisi iliyotolewa chini yake, kulitokana na sababu yoyote isiyoepukika kutachukuliwa kuwa si ukiukwaji wa masharti hayo. |

JEDWALI

**<u>JEDWALI LA KWANZA</u>**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1) na 6(2))*

**Fomu ya Kuomba Kibali cha Watoa Huduma**

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

Jina la kampuni…………………………………………………………………..…………………….

Anwani……………………………………………………………………………………………….

Mkoa,…………………………………………………………………………………………………

Nambari ya simu………………………………………………………………………………………….………

Barua pepe……………………………………………………………………………..……………………

1. **Maelezo ya Mawasiliano**

   i. Jina la mwombaji:..................................................................................
   ii. Nafasi/Cheo:............................................................................................
   iii. Anwani:.....................................................................................................
   iv. Nambari ya simu:....................................................................................
   v. Barua pepe:...............................................................................................

2. **Taarifa za Kampuni:**

   i. Anwani ya Biashara:...............................................................................
   ii. Usajili wa Kampuni/Nambari ya Utambulisho:........................…...............
   iii. Tarehe ya usajili:.......................................................................................

3. **Huduma inayoombwa:**

   i. Huduma inayoombwa:……………………………………..…………………………
   ii. Njia Zitakazotumika:………………………………………………………………………..
   iii. Vituo Vitakavyohudumiwa:…………………………………………………………………
   iv. Idadi ya safari:……………………………………………………………………….
   v. Tarehe ya kuanza kutoa huduma:………………………..……………………………
   vi. Mahitaji yoyote Maalum …………………..:…………………………………….

4. **Nyaraka ambatishwa;**

   Ambatisha nyaraka zinazohitajika kwa ajili ya maombi ya kibali (kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 4(2)

5. **Ada ya Maombi** ………………………………………(ilipwe kupitia nambari ya kumbukumbu ya malipo)

6. **Tamko**

Mimi ………………………………………………. Nakiri kwamba, maelezo yaliyotolewa katika maombi haya ni ya kweli, sahihi, na kamili kwa kadri ya ufahamu wangu. Ninaelewa kwamba kutoa taarifa zozote za uongo kunaweza kusababisha kukataliwa kwa ombi hili au kubatilishwa kwa kibali.
Sahihi ya Mwombaji: ______________________________________ Tarehe: _________________

**MAOMBI YA LESENI YA KUTOA HUDUMA YA RELI**

(*Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 6(2)*)

Jina la Kampuni ya Mwombaji: …………………………………………………

Nambari ya usajili: …………………………….……………………………………

Nambari ya Kibali cha Msimamizi wa Miundombinu: ……………………………..

Tarehe ya Kutolewa: …………………………………………………..………………

Mahali kampuni Iliposajiliwa : ………………………………………..…………

Anwani ya Mahali ilipo: ……………………………………………………………………

Anuani ya posta: …………………………………………………………..…….

Nambari ya simu: ……………………………………………………………

Barua pepe: ……………………………………………

**Jedwali la Maelezo ya Umiliki wa Hisa:**

| Jina | Uraia | Anwani | Asilimia |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**AINA YA LESENI INAYOOMBWA**

| SN | Aina ya Huduma Inayotolewa | Chagua |
|---|---|---|
| 1 | Huduma za Abiria | |
| 2 | Huduma ya treni za abiria mjini | |
| 3 | Huduma za Mizigo | |

Maelezo ya huduma zitakazotolewa kwa kifupi:

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

Maelezo ya Leseni iliyopita (kama ipo). Nambari ya leseni……………………tarehe……………….………

Maelezo ya jumla ya mwombaji juu ya rasilimali za kifedha (Ambatisha kurasa za ziada kama zitahitajika).
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

Mimi ………………………………….. Ninakiri kwa ufahamu na imani yangu kwamba taarifa zote zilizomo katika maombi haya ni za kweli na sahihi.

Jina Kamili: ………………………………………………………………………………

Cheo: ………………………………………………………………………………

Sahihi: ……………………………………………………………………………

Muhuri: ……………………………………………………………………………..
Tarehe: …..………………………………………

**JEDWALI LA PILI**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5 na 7))*

**MAOMBI YA KIBALI**

| AINA YA HUDUMA | ADA YA MAOMBI | ADA YA KIBALI |
|---|---|---|
| HUDUMA YA ABIRIA | US$.....(au sawa na TZS) | US$.....(au sawa na TZS) |
| HUDUMA YA MIZIGO | US$......(au sawa na TZS) | US$......(au sawa na TZS) |

**MAOMBI YA LESENI**

| AINA YA HUDUMA | ADA YA MAOMBI | ADA YA LESENI |
|---|---|---|
| HUDUMA YA ABIRIA | US $ 100 $.....(au sawa na TZS) | US $ 2000 $.....(au sawa na TZS) |
| HUDUMA YA MIZIGO | US $ 100 $.....(au sawa na TZS) | US $ 4000 $.....(au sawa na TZS) |
| | | |

**JEDWALI LA TATU**

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 10 na 14)*

**STAHIKI ZA MTOA HUDUMA**

**1.** kiwango cha chini cha huduma ya miundombinu kinachorejewa katika kanuni ya 10(1) kitajumuisha haki ya kutumia Miundombinu kama ilivyotolewa na hasa-

(i) haki ya kutumia sehemu za vigeuza njia na makutano kama inavyohitajika kutumia uwezo wa njia husika;

(ii) udhibiti wa treni, ikijumuisha ishara na mawasiliano na utoaji wa taarifa juu ya mwenendo wa treni; na

(iii) taarifa nyingine zote kama zitakavyohitajika katika kutekeleza au kuendesha huduma ambayo uwezo umetolewa.

**2.** Uwezo wa kufika kwenye vituo vya huduma na usambazaji zilizorejewa katika kanuni ya 10(1) na (4) itajumuisha pamoja na-

(a) matumizi ya vifaa vya usambazaji wa umeme;

(b) vituo vya kujazia mafuta

(c) vituo vya abiria, ikiwa ni pamoja na majengo na vifaa vingine;

(d) vituo vya kusafirisha mizigo;

(e) eneo la kupanga treni;

(f) njia za mchepuko; na

(g) Sehemu za matengenezo na vifaa vingine vya kiufundi.

**3.** Huduma za ziada zinazorejewa katika kanuni ya 10 (4) zitajumuisha-

(a) umeme;

(b) usambazaji wa mafuta, kupanga behewa na huduma zingine zote zinazotolewa katika vifaa vya huduma za ufikiaji zilizorejewa katika aya ya (2);

(c) mikataba midogomidogo kwa ajili ya-

i. udhibiti wa usafirishaji wa bidhaa hatari; na

ii. usaidizi katika kuendesha treni zisizo za kawaida.

**4.** Huduma za ziada zinazorejewa katika kanuni ya 10(4) zinaweza kujumuisha:

(a) upatikanaji wa mtandao wa mawasiliano;

(b) utoaji wa taarifa za ziada; na

(c) ukaguzi wa kiufundi wa vitembea reli.

## JEDWALI LA NNE

*(Iimetengenezwa chini ya Kanuni ya 14)*

## TOZO ZA MIUNDOMBINU

### 1. Misingi ya malipo ya utoaji huduma

(a) Msimamizi wa miundombinu atahakikisha kwamba matumizi ya mpango wa tozo-

i. yanazingatia taratibu zilizowekwa katika taarifa ya mtandao iliyoandaliwa kwa mujibu wa kanuni ya 13; na

ii. ni sawa kwa shughuli tofauti za reli zinazotoa huduma sawa katika sehemu sawa ya soko.

(b) ukokotoaji wa ada utazingatia umbali, muundo wa treni na mahitaji yoyote maalum kulingana na mwendo kasi, ekseli na kiwango au muda wa matumizi ya miundombinu.

(c) isipokuwa pale ambapo mipango mahususi inafanywa, msimamizi wa miundombinu atahakikisha kwamba mfumo wa utozaji unaotumika unatokana na kanuni sawa katika mtandao wake wote.

(d) tozo ya mindombinu iliyoainishwa katika aya ndogo ya (a) na (b) ya Jedwali hili zitazingatia ghrama za moja kwa moja zilizoingiwa katika uendeshaji wa treni.

(e) katika kupangilia mfumo wa tozo wa utoaji wa huduma zilizorejewa katika aya ya (5), msimamizi wa miundombinu atazingatia hali ya ushindani wa usafiri wa reli.

(f) ada ya kutumia miundombinu inaweza kujumuisha malipo ya msongamano wa sehemu itakayokuwa imetambulika.

(g) gharama zinazorejewa katika aya ndogo ya (4) zinaweza kukadiriwa kulingana na huduma za treni, muda na gharama za miundombinu inayohusika.

### 2. Utofauti katika misingi ya utozaji

(a) Ili kufidia gharama zilizotumika, Mdhibiti atamuidhinisha msimamizi wa miundombinu chini ya ukaguzi wa gharama za upatikanaji kufanya marejeo ya tozo, kulingana na ufanisi, uwazi na kutokubagua, huku akihakikisha ushindani bora wa usafirishaji wa kimataifa.

(b) Bila ya kujali masharti ya aya ndogo ya (1) msimamizi wa miundombinu atajumuisha matumizi ya miundombinu ya sehemu ya soko ambayo yanaweza kulipa angalau gharama ya moja kwa moja iliyopatikana kutokana na uendeshaji wa huduma ya reli, pamoja na kiwango cha mapato ambacho soko linaweza kubeba.

3. **-**(1) Kwa miradi mahususi ya uwekezaji iliyokamilishwa kufuatia kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, msimamizi wa miundombinu anaweza kuweka gharama kwa msingi wa gharama za muda mrefu za mradi.

(2) Mpangilio wa utozaji katika aya ndogo ya (1) utajumuisha makubaliano ya kugawana hatari kwa uwekezaji mpya.

**4.-** (1) Gharama za wastani na za ziada za msimamizi wa miundombinu kwa matumizi sawa ya miundombinu yake lazima ziwe huduma zinazoweza kulinganishwa katika sehemu ya soko moja kwa kutegemea gharama sawa.

(2) Taarifa ya mtandao inayotolewa na msimamizi wa miundombinu itaonyesha kuwa mfumo wa utozaji unakidhi mahitaji katika aya ya (1) na kufanywa bila kufichua taarifa za siri za kibiashara za mtoa huduma.

**5.** Ikiwa msimamizi wa miundombinu anakusudia kurekebisha vipengele muhimu vya mfumo wa tozo uliorejewa katika aya ya 2 atafanya marekebisho hayo na kuyatangaza angalau miezi mitatu kabla.

**Punguzo**

**6**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 14 na aya ya 1(d) ya Jedwali hili, punguzo lolote kwenye tozo anazotoza msimamizi wa miundombinu, kwa huduma yoyote lazima lizingatie kanuni zilizoainishwa katika aya hii.

(2) Isipokuwa pale aya ndogo ya (3) inatumika, punguzo litawekwa tu katika uokoaji halisi wa gharama ya usimamizi kwa msimamizi wa miundombinu na, katika kuamua kiwango cha punguzo hakuna kiwango cha tozo kitakachopunguzwa katika tozo iliyokwishawekwa.

(3) Msimamizi wa miundombinu anaweza kuanzisha mifumo inayopatikana kwa watoa huduma kwa kuzingatia mtiririko maalum wa usafirishaji, kutoa punguzo la muda ili kuhimiza maendeleo ya huduma mpya za reli, au kuhimiza matumizi ya njia zisizotumika kwa kiasi kikubwa.

(4) Punguzo linalopatikana litakuwa kwa mujibu wa mapitio ya gharama za huduma.

(5) Punguzo linaweza tu kuhusiana na gharama zinazotozwa kwa sehemu maalum ya miundombinu.

(6) Mipango sawa ya punguzo lazima itumike kwa huduma zinazofanana.

Dodoma
…………………………, 2023

**MAKAME MNYAA MBARAWA**
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*